MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Sababu za Matumizi ya Vipashio vya Lugha vya Kimamlaka na Kiitikadi Katika Midahalo ya Kisiasa ya 2022 Nchini Kenya Kupitia Youtube: Mtazamo wa Uchanganuzi wa Kidiskosi

Nelson Asige[a*], Fridah Miruka[a], Juliet Jagero[b]

Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Sanaa na Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya.

Idara ya Isimu, Lugha na Fasihi, Shule ya Elimu, Binadamu na Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Bondo, Kenya.

**IKISIRI**

Makala hii inachunguza sababu za matumizi ya vipashio vya lugha vya kimamlaka na kiitikadi katika midahalo ya kisiasa ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2022 nchini Kenya kupitia jukwaa la YouTube. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kubainisha namna na sababu zilizowafanya wanasiasa kutumia lugha yenye vipashio vya mamlaka na itikadi katika diskosi zao za kisiasa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi (UHU) inayobainisha uhusiano kati ya lugha, mamlaka na itikadi katika jamii. Muundo wa utafiti uliotumika ulikuwa wa kiuchanganuzi wenye mkabala wa kiuthamano. Eneo la utafiti lilikuwa katika midahalo ya kisiasa ya uchaguzi wa 2022 nchini Kenya; iliyopatikana katika jukwaa la kidijitali la YouTube. Idadi lengwa ya utafiti ilikuwa midahalo ya wanasiasa wakuu kutoka mirengo ya kisiasa ya Azimio la Umoja na Kenya Kwanza iliyohusisha kampeni za uchaguzi huo. Data zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ambapo video za midahalo zenye maudhui yanayodhihirisha matumizi ya vipashio vya mamlaka na itikadi zilichaguliwa kama sampuli ya utafiti. Data zilikusanywa kupitia uchunguzi wa nyaraka za kidijitali (video za YouTube), kisha zikachanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo kwa kuongozwa na misingi ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa wanasiasa walitumia vipashio vya lugha vya kimamlaka na kiitikadi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kufichua siri za kisiasa za wapinzani, kuwalaumu wapinzani kwa matatizo ya kijamii na kiuchumi, kutoa ahadi kwa wananchi, kuwapa wananchi matumaini, kuchochea dhidi ya wapinzani na kufanikisha propaganda za kisiasa. Kwa ujumla, utafiti umeonyesha kuwa lugha ya kisiasa hutumiwa kimkakati kama nyenzo ya kudhihirisha mamlaka na kuendeleza itikadi za kisiasa kwa lengo la kushawishi mitazamo na maamuzi ya wapiga kura.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Itikadi,
Malumbano,
Mamlaka,
Siasa,
Uchaguzi.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 2 Februari 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 17 Machi 2026
Tarehe ya Kukubalika: 23 Machi 2026
Mtandaoni: 24 Aprili 2026

## 1. Utangulizi

Kazi Itikadi na mamlaka ni dhana mbili ambazo huambatana katika asasi ya siasa. Dhana hizi mbili huwa na mwingiliano, huku itikadi ikiongoza katika kudhihirika kwa mamlaka. Mamlaka na itikadi hudhihirika kupitia matumizi ya lugha, na huwezesha wananchi kutathmini kiongozi watakaomchagua. Fairclough (1989), anaeleza kuwa katika ushindani wowote wa kisiasa, hamna budi kudhihirika kwa miundo fulani ya kiuwezo na nguvu, ambayo husababishwa na itikadi, kwa lengo fulani. Mamlaka ni uwezo wa kushawishi au kuelekeza matendo, imani, mielekeo au mienendo ya watendaji fulani. Hairejelei matumizi ya nguvu au masharti ya mhusika mmoja dhidi ya wengine, bali huelekezwa kwa njia isiyo wazi. Mahusiano ya mamlaka huathiri ushiriki wa kisiasa kwa kuwafanya baadhi ya watendaji, hususan wanasiasa, kuonekana kuaminika huku wengine, hasa wapinzani, kuonekana wasiofaa. Hivyo, baadhi ya watendaji na mitazamo yao wanaweza kuachwa bila uhalali wowote kutokana na mahusiano ya kimamlaka. Kwa upande mwingine, itikadi hurejelea imani ya mtu au kikundi fulani. Mawazo ya kiitikadi ndiyo huamua siasa, washindi na wanaoshindwa. Uamuzi wowote wa kisiasa ni wazo na hufuata itikadi. Wanasiasa huwa na wakati mgumu wa kuwashawishi wananchi kuwachagua wakati mawazo yao

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: naasige@gmail.com.

Mhariri: Leonard Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Nukuu: Asige N., Miruka F., & Jagero J. (2026). Sababu za Matumizi ya Vipashio vya Lugha vya Kimamlaka na Kiitikadi Katika Midahalo ya Kisiasa ya 2022 Nchini Kenya Kupitia Youtube: Mtazamo wa Uchanganuzi wa Kidiskosi. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 40 – 49. https://doi.org/10.61889/4zbzx888.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

hayaambatani na itikadi maarufu au iliyoimarishwa vyema. Fairclough (kht) anachagiza kuwa wakati dhana hizi mbili zinadhihirika katika matumizi ya lugha ya wanasiasa, huonyesha sababu fulani au lengo la wanasiasa hawa. Utathmini huu wa Fairclough (1989), kuhusiana na dhana za mamlaka na itikadi, na sababu za kudhihirika kwa mamlaka na itikadi, zilichangia makala hii ambayo ilihakiki sababu za wanasiasa kutumia mamlaka na itikadi katika midahalo yao ya siasa za 2022 nchini Kenya. Uchaguzi mkuu wa 2022 nchini Kenya ulikuwa tofauti kabisa na chaguzi za awali, kwani ulidhihirisha ushindani mkubwa na wa aina ya kipekee kutoka kwa wanasiasa Raila Odinga wa mrengo wa Azimio la Umoja na William Ruto wa Kenya Kwanza.

Wawili hawa walikuwa na ushawishi mkubwa nchini, huku mikutano yao ya kampeni ikivutia lukuki ya wananchi. Uchaguzi huu ulikuwa wa kipekee kwani ulidhihirisha ushindani wa urais kati ya Naibu wa rais dhidi ya Waziri mkuu wa zamani; ambaye aliungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta dhidi ya Naibu wake, hivyo kusababisha uhasama wa kisiasa, jambo lililofanya midahalo yao kuwa angavu na yenye kuvutia, huku maswala nyeti yakiwasilishwa hadharani kwa njia wazi na fiche. Wapinzani hawa wawili waliongozwa na misukumo mbalimbali katika midahalo yao. Makala hii ilinuia kudhihirisha kuwa wawaniaji hawa wawili, pamoja na wanasiasa katika mirengo yao, walipotumia lugha, walikuwa na misukumo, na hivyo kuzungumza kwa sababu na nia maalum.

## 2. Msingi wa Nadharia.

Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi (U.H.U). Uchanganuzi hakikifu wa usemi una historia ambayo inaweza kufuatiliwa kutoka miaka ya 1970 na 1980. Baadhi ya waasisi wake ni pamoja na Fairclough (1989, 1993, 2001, 2003), Kress (1990, 2003), Wodak (2001, 2004, 2009) na Van Dijk (1998). Van Dijk (1998), anahoji kuwa nadharia hii ni fani inayojihusisha na uchanganuzi wa diskosi, andishi na semi, ili kufichua vyanzo na misingi ya mamlaka, udhibiti, usawa, utousawa na upendeleo. Uchanganuzi hakikifu wa usemi hufafanuliwa kama taaluma pana ambayo hutumia mbinu tofauti kutathmini asasi mbalimbali za kijamii, kisiasa na kadhalika. Hurejelea uchunguzi wa aina mbalimbali za diskosi zenye uhusiano na asasi na miktadha mbalimbali za kijamii na kisiasa, kwa kuzingatia jinsi mamlaka ya kijamii, uwezo, nguvu, udhibiti na utousawa hutekelezwa, kutolewa tena na wakati mwingine kupingwa.

Kwa mujibu wa Norman Fairclough (1989), diskosi inarejelea mchakato mzima wa mwingiliano ambao usemi au maandishi ni sehemu tu. Nao Brown na Yule (1983), wanaeleza kuwa uchanganuzi wa diskosi ni jumla ya uchunguzi wa uamilifu wa lugha. Uzalishaji wa mamlaka na udhibiti, zinazodhihirika kupitia matumizi ya lugha, ndio jambo muhimu zaidi katika nadharia hii ya U.H.U, kwa mujibu wa Wodak (1996). Lugha inachukuliwa kuwa tendo la kijamii linaloendeshwa kiitikadi. Diskosi inatathminiwa kama milki ya kijamii inayomiliki nguvu kupitia lugha tumizi mahsusi. Nadharia hii inalenga kuonyesha uhusiano kati ya lugha na itikadi. Uchanganuzi hakikifu wa usemi hufichua uhusiano wa kimazungumzo na miundo mipana ya kijamii na kitamaduni inayoundwa kiitikadi ili kudhihirisha mahusiano ya kimamlaka na mapambano ya kupata mamlaka hayo. Mamlaka, kidiskosi, hudhihirishwa zaidi kupitia matumizi ya lugha, huku ikilenga kudhibiti na kuathiri kikundi fulani kitabia na kimielekeo. Katika utafiti huu, nadharia hii ilihusika katika kufafanua matini, kufasiri michakato na maingiliano yake pamoja na kueleza jinsi michakato hiyo inavyohusiana na tendo la jamii. Baadhi ya mihimili ya nadharia hii iliyofanikisha makala hii ilitathmini lugha kama msimbo unaomiliki na kudhihirisha uwezo, wenye uwezo wa kuzingatia matatizo ya kijamii na wenye maana katika kipindi fulani cha kihistoria.

## 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifuata muundo wa kiuchanganuzi kwa mkabala wa kiuthamano, kwa kuwa ulilenga kuchunguza na kufasiri matumizi ya vipashio vya lugha vya kimamlaka na kiitikadi katika diskosi za wanasiasa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2022 nchini Kenya. Eneo la utafiti lilikuwa katika majukwaa ya mawasiliano ya kisiasa yaliyorekodiwa na kupakiwa katika mtandao wa YouTube, ambapo hotuba na midahalo ya wanasiasa wa Kenya wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2022 zilipatikana.

Idadi lengwa ya utafiti ilikuwa midahalo na hotuba za wanasiasa waliokuwa wakishiriki katika kampeni za uchaguzi mkuu tajwa, hasa wale waliokuwa katika mirengo mikuu ya kisiasa ya Azimio la Umoja na Kenya Kwanza. Midahalo hii ilijumuisha hotuba za hadhara, mikutano ya kampeni pamoja na mawasiliano ya kisiasa yaliyokuwa yamehifadhiwa katika mfumo wa video. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika katika uteuzi wa data, kwa kuwa mtafiti alichagua kimakusudi video za midahalo ya kisiasa zilizodhihirisha matumizi ya vipashio vya mamlaka na itikadi katika lugha ya wanasiasa. Kupitia mbinu hii, sampuli ya utafiti ilijumuisha video teule za hotuba na midahalo ya wanasiasa waliokuwa wakishiriki katika kampeni za uchaguzi tajwa ambazo zilikuwa na maudhui yaliyofaa kwa madhumuni ya utafiti.

Ukusanyaji wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchunguzi wa nyaraka za kidijitali, ambapo video za midahalo ya kisiasa zilipakuliwa au kutazamwa kutoka kwenye jukwaa la YouTube na kisha kunukuliwa sehemu muhimu za diskosi zilizokuwa na matumizi ya vipashio vya mamlaka na itikadi. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo kwa kuongozwa na misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi, ambapo matini za diskosi zilizokusanywa zilichambuliwa ili kubainisha sababu na mikakati ya kisiasa iliyosababisha matumizi ya vipashio vya mamlaka na itikadi katika hotuba za wanasiasa. Hatimaye, uwasilishaji wa data ulifanywa kwa njia ya kinathari, ambapo dondoo za diskosi kutoka kwa wanasiasa zilinukuliwa na kufafanuliwa kwa kina ili kuonyesha namna vipashio vya mamlaka na itikadi vilivyotumiwa pamoja na maana zake katika muktadha wa siasa za uchaguzi wa mwaka 2022 nchini Kenya.

### 3.1. Mapitio ya Maandishi

Mtaalamu Bevir (1999), anatathmini maoni ya mwanahistoria wa Kifaransa, Faucault (1926-1984), kwamba dhana ya mamlaka ni muhimu sana katika siasa, kwani humsaidia mwanasiasa kwa kumjengea hulka binafsi. Katika hali hii, husaidia katika jinsi mwanasiasa fulani anajiona na kujitathmini mwenyewe pamoja na mahusiano yake na wengine. Katika kufanya hivi, wananchi wapigaji kura hufanya uamuzi rahisi wa kumchagua kwani ana matakwa yanayomridhisha yeye binafsi pamoja na jamii pana inayomzingira. Katika maisha ya wengine, hudhihirisha mabadiliko chanya yenye athari nzuri kwa kuwa mwanasiasa fulani ametumia hulka yake vyema katika kujenga jamii hiyo. Maoni ya Faucault ni muhimu katika utafiti huu kwa kuhusika na sababu mojawapo ya matumizi ya vipashio vya mamlaka na itikadi, ambayo ni ujenzi wa hulka ya mwanasiasa.

Kwa mujibu wa Fairclough (2003), maneno ya lugha ndiyo yanaipa lugha nguvu. Wanasiasa wanapotumia lugha, huchagua maneno ya lugha kistadi ili kudhihirisha jukumu la lugha la kudhihirisha mamlaka. Kwa sababu hii, ikizingatiwa kuwa mamlaka hulenga kuonyesha usawa na utousawa kati ya makundi ya kijamii, wale wanaoonewa kwa kuibuka kwa utousawa hujaribu kulalamikia hali mbalimbali ambazo zilisababishwa na wapinzani wao au watendaji fulani katika harakati za kushindania mamlaka, kupitia lugha na matumizi yake. Katika kutoa lalama hizi, lugha hujidhihirisha kama chombo cha kubadilisha mielekeo ya wenye maamuzi kumwelekea mwanasiasa fulani, hivyo kubadilisha nia ya wengi katika kurudhisha matakwa ya wachache. Maoni haya ya Fairclough (1989), ni nguzo katika makala hii ambayo vilevile imetalii nafasi ya lugha katika kudhihirisha lalama za wanasiasa kwa wapinzani wao wakilenga kujivutia mamlaka huku wapinzani wakitwazwa na kunyanganywa mamlaka.

Fairclough (2006), anadhihirisha nafasi ya diskosi katika kudhihirisha hali halisi. Katika muktadha huu, hali halisi hudhihirishwa kupitia matumizi ya lugha kwa njia ya kuweka mambo ya siri kuwa wazi. Aghalabu, wanasiasa wanaofanya hivi hulenga kutoboa siri fulani kuhusu mapungufu ya wapinzani wao kwa nia ya kujivutia mamlaka na kuwafanya wananchi kuwachagua kidemokrasia. Baadhi ya diskosi za utafiti huu zilidhihirisha sababu hii ya wanasiasa kutumia mamlaka na itikadi.

Patton (2002) vilevile anaangazia dhima ya lugha ya siasa katika kunyosha kidole cha lawama kwa wapinzani huku hulka ya mwanasiasa ikijengwa. Anaeleza kuwa mwanasiasa hana budi ila kujivutia mamlaka kwa vyovyote vile, ata ikibidi kudhihirisha utousawa kupitia kuwatilia doa washiriki fulani wa kisiasa, huku akijikuza kwa wakati huo kama suluhu kwa mapungufu yaliyosababishwa na wapinzani. Maoni ya Patton (2002), yaliwiana na yale ya Fairclough (2003), katika kudhihirisha utousawa katika diskosi kupitia lawama. Makala hii imetalii sababu ya wanasiasa kutumia vipashio vya mamlaka na itikadi ili kukuza hadhi, hivyo kufaidi kwa maoni ya Patton (2002).

Lugha hulazimu utiifu wa matakwa, hasa katika uhusiano wa mwanasiasa na hadhira yake. Kupitia lugha, uwezo wa mwanasiasa hubadilika na kuwa haki, kwa hivyo kusababisha utiifu kutika kwa hadhira yake. Hii ndiyo sababu ya hadhira kutathmini kila kitu asemacho mwanasiasa kuwa cha kweli, huku uaminifu ukifuata. Edelman (1977), anahoji zaidi kuwa hali ya kumtii mwanasiasa hubadilika na kuwa wajibu, hivyo kuongeza matarajio ya hadhira ya mwanasiasa kwa mwanasiasa huyo, na wa aidha kuzidisha matarajio ya mwanasiasa katika kupata mamlaka yanayoshindaniwa. Hivi ni kumaanisha kuwa, utiifu unaobadilika na kuwa wajibu ni muhimu kwa mwanasiasa katika kujivutia udhibiti. Utafiti huu ulitalii baadhi za diskosi za wanasiasa katika siasa za uchaguzi mkuu wa 2022 nchini Kenya zilizoonyesha udhibiti uliosababisha utiifu na uwajibikaji.

Jones na Peccei (2004), wanachagiza kuwa nguvu za lugha zinapodhihirika kupitia matumizi yake, udhibiti hudhihirika. Udhibiti huu unaweza kuwa wa: kifikra, kimaadili, kimielelekeo, kisaikolojia na kadhalika. Kwamba, matumizi ya lugha ya mwanasiasa ni muhimu kwa kiasi kikubwa kuchangia badiliko katika hadhira yake. Kwa sababu hii, wanasiasa huchunza maneno ya lugha, huyatengeneza na kuyafanya yawe na athari kubwa kwa hadhira zao, hivyo kusababisha athari na mabadiliko kati ya hadhira zao. Utafiti huu ulitalii baadhi ya midahalo ya siasa za 2022 ili kudhihirisha namna mamlaka na itikadi ilitumiwa kwa nia ya kuathiri maadili na mielekeo ya wapiga kura.

## 4. Matokeo

Katika kutathmini sababu za wanasiasa kutumia vipashio vya mamlaka na itikadi katika midahalo ya siasa za uchaguzi wa 2022 nchini Kenya, makala hii ilichanganua sababu zifuatazo;

### 4.1. Kuibua tetesi za kisiasa

Utafiti huu ulibaini kuwa mojawapo kati ya sababu za wanasiasa kutumia mamlaka na itikadi katika midahalo yao ya siasa za uchaguzi mkuu wa 2022 ilikuwa ni kufichua siri za kisiasa za wapinzani wao ambazo hazikuwa zimewekwa hadharani hapo awali. Walifanya hivi kwa nia ya kuwatwaza wapinzani wao huku wakijijivutia mamlaka upande wao. Utafiti ulibaini kuwa siri zilizofichuliwa zilikuwa zile za matendo yasiyofaa, ili wananchi wawatathmini wapinzani kama watu wasiofaa, hivyo kuwaunga mkono wasemaji wa habari hizo. Utafiti huu ulinufaikia maoni ya Ku (1998), ambaye alihoji kuwa wanasiasa aghalabu hufichua siri za wapinzani wao hadharani ili kufanya hadhira zao kuwachukia warejelewa. Kwa kuwa siasa ni asasi ya maslahi, wanasiasa hujielekeza wanakoona mamlaka, hivyo huweza kushirikiana na wakati mwingine kutengana. Kwa sababu hii, huweza kujua mengi kuhusu wanasiasa wengine, na hivyo wanapojipata kuwa wapinzani, hueleza baadhi ya siri na kufichua hali halisi ambazo zisingejulikana iwapo wangekuwa pamoja kiitikadi. Isitoshe, siri mbaya hufichuliwa ili wanasiasa fulani wasichaguliwe au wachukiwe, hivyo kugeuza mkondo wa mamlaka kwa njia isiyo wazi, uwaendee wenye ufichuzi wa siri zile. Mfano ufuatao wa mwanasiasa Rigathi

Gachagua alipokuwa akikampeni kule Nyeri unadhihirisha hali hii;

Dondoo 1: Msemaji 1

> …Mimi Rigathi Gachagua nimekusaidia miaka ishirini, wewe nilikutoa kwa bar, nikakuunda mpaka ukakua Rais… Sasa baada ya kufanya hiyo yote unatisha mimi ati nitajua wewe ni rais…bora tu usituue vile baba yako aliua J.M Kariuki…
> https://youtu.be/L2gQ_tvDJC0?si=uogMDCt6o9x_C_eZ.
> *Tarehe 30 Julai, 2022.*

Katika diskosi hii, msemaji anafichua kuwa kama isingekuwa yeye, basi Uhuru Kenyatta asingeweza kuwa rais wa Kenya hapo mbeleni; kwani yeye ndiye aliyemtoa kwenye bar na kumuunda kiasi cha kuwa Rais. Katika diskosi hii, msemaji anatumia itikadi kali kufichua hali halisi ya mpinzani wake, na aliyekuwa Rais wa wakati huo, Uhuru Kenyatta. Katika uchaguzi wa 2022, Rais Uhuru Kenyatta alimuunga mkono Raila Odinga, hivyo kuleta upinzani kutoka kwa waandani wake wa karibu wa hapo awali alokuwa nao katika chama cha Jubilee. Mmoja kati ya wale waliompinga sana ni msemaji, Rigathi Gachagua. Fairclough (2006), anahoji kuwa maoni yenye nguvu kutoka kwa wapinzani kuhusu hali halisi huweza kubadilisha mielekeo ya wapiga kura kumhusu mlengwa. Katika muktadha huu, msemaji, ambaye alikuwa ameteuliwa kuwa mgombea mwenza wa William Ruto katika mrengo wa Kenya Kwanza, alijiweka katika nafasi kubwa kisiasa ya kuweza kumuunda Kenyatta hadi kuwa Rais. Kwa njia hii, anajivutia mamlaka na kujitia katika upeo wa juu zaidi.

Vilevile, msemaji anafichua suala ambalo lilikuwa nyeti na lenye uwezo mkubwa wa kuleta mitafaruku ya kisiasa kwa kujionyesha kama mwenye ujuzi wa aliyemuua mwanasiasa J.M. Kariuki, mwaka wa 1975. Anamwonya rais kuwa asiwaue jinsi babake, Jomo Kenyatta alivyomuua mwanasiasa huyo. Kwa kuwa diskosi ni sehemu ya historia ya kijamii (Wodak, 1996), utafiti ulitalii historia ya J.M. Kariuki. Harms (2021), anachagiza kuwa mwanasiasa huyu alikuwa mpinzani mkubwa sana wa serikali ya Jomo Kenyatta, kwa kulaumu hali ngumu ya maisha iliyowakumba wakenya katika wakati huo wa kihistoria kwa kuwepo kwa serikali ambayo haikuwajali. Harms (2021), anaeleza kuwa kwa mara si haba, Kariuki alilalamikia hali mbaya ya kuwepo kwa mamilionea wachache kati ya mamilioni ya wananchi. Hali hizi ziliwafanya Kariuki na Jomo Kenyatta kuwa mahasimu wa kisiasa, na ingawa hakuna ithibati tosha inayomhukumu Jomo Kenyatta kuwa muuaji wake Kariuki, wengi walidhani hivyo. Kwa kusema haya, msemaji wa diskosi hii anajitokeza kuwa shujaa mjuzi ambaye alikuwa anawafichua wauwaji na maadui wa taifa la Kenya. Vilevile, kwa kutoa madai haya, msemaji alilenga kuwafanya wananchi wa Nyeri kumhusudu Uhuru Kenyatta kwa kutoka katika familia ya wauaji; na kuweza kuwa muuaji mwenyewe, na kuepukana na matakwa yake ya kuwataka wamchague Raila Odinga, hivyo kujiegemeza katika mamlaka, yeye pamoja na mrengo wake.

Mbali na diskosi hii, ufichuzi wa hali halisi vilevile unabainika kupitia diskosi ya William Ruto katika kumbukizi mojawapo aliyowatolea hadhira yake katika mojawapo ya mikutano yake ya kisiasa;

Dondoo 2: Msemaji 2

> …Unajua tulienda kufanya uchaguzi, tukashinda…. baadaye mlango ikakuwa wazi wengine wakaingia ndani wakaharibu…. Mimi nikatoka hapa nikafika Statehouse…nikakuta rafiki yangu ako hapo, sitaki kusema alikuwa anafanya nini … "mimi nataka kwenda Ichaweri" …Mimi nikamwangalia nikamwambia wewe! Ni vile tu nilikuwa na heshima ningemchapa Kofi…
> https://youtu.be/qQvJMtUdcy4?si=wN-1700pul0zcrp7.
> *Tarehe 4 Julai, 2022.*

Katika diskosi hii, msemaji anaonekana kufichua siri ya mkutano uliofanyika kati yake na Uhuru Kenyatta baada ya uchaguzi wa 2017 kutupiliwa mbali na Mahakama Kuu kama iliyokosa haki na uaminifu kupitia wizi wa kura. Msemaji anaeleza kuwa alipoenda katika ikulu, alimpata Kenyatta ambaye alikuwa radhi kurudi nyumbani kwa kushangazwa na maamuzi ya korti hiyo. Msemaji anajikuza kama suluhu katika wakati mgumu anapojitokeza kuwa sababu za Uhuru Kenyatta kubadilisha nia yake ya kufa moyo na kuongoza kampeni za marudio ya uchaguzi ili aweze kushinda katika awamu hiyo ya pili. Msemaji anaeleza kuwa alitaka kumpiga rais kofi kwa kutaka kufa moyo. Hii ni siri ambayo ilikuwa kati ya wawili hawa katika mkutano huo wa faragha, ila inajitokeza hadharani kati ya wananchi. Katika hali hii, anayejitokeza kuwa alikuwa na ushawishi mkubwa pamoja na nguvu katika wakati huo alikuwa msemaji, bali si rais. Kutoa madai kuwa alitaka kumpiga rais kofi kulimkuza na kumpa mamlaka kati ya wananchi kwa njia iliyokuwa fiche. Kwa namna hii, alionekana kama mwenye msimamo dhabiti, na aliyekuwa radhi kulinda mamlaka kwa vyovyote vile, ingawa ingembidi ampige rais kofi. Vilevile, kati ya wananchi, Uhuru Kenyatta alionekana kama asiyekuwa na uwezo, hivyo kupuuziliwa mbali pamoja na mgombea kiti cha urais katika mrengo wa Azimio la Umoja, Raila Odinga.

### 4.2. Kuwalaumu wapinzani

Utafiti huu ulibainisha lawama za kisiasa kama sababu za wanasiasa kutumia mamlaka na itikadi za kisiasa katika midahalo yao ya siasa za 2022 nchini Kenya. Lawama hizi zilielekezewa wapinzani kwa nia ya kuwadokeza kama wasiowajali wananchi, na kwamba wao ndio waliofaa kulaumiwa kwa sababu ya masaibu yaliyowakumba wakenya katika kipindi hicho cha kihistoria. Miaka ya baada ya 2020, baada ya janga la UVIKO-19, ilishuhudia hali nyingi hasi zilizowakumba wakenya. Monge & Lazacano (2022), wanaangazia baadhi ya kadhia zilizozuka kwa sababu ya janga la UVIKO-19. Wanaeleza kuwa kulishuhudiwa ongezeko la bei ya bidhaa na huduma muhimu duniani. Baadhi ya wanasiasa walitumia fursa hii kutoa lawama kwa serikali ya Uhuru Kenyatta, ambaye alimuunga mkono Raila Odinga wa Azimio la Umoja, ili kuwadhihirisha kuwa sawa, na kwamba kumchagua Raila Odinga kama rais wa Kenya

hakukuwa tofauti na utawala wa Uhuru Kenyatta, ambao kwa mujibu wa wapinzani, uliwaongeza dhiki wananchi kwa kiasi kikubwa. Kwa kuwa mamlaka hufungamana na hali mbalimbali za kijamii za wakati fulani wa kihistoria (Van Dijk, 1984), wengi wa wanasiasa waliotumia fursa ya kuwepo kwa UVIKO-19 ili wafanikishe lawama zao. Wakati uo huo, wanasiasa walijiepushia lawama katika harakati za kuwalaumu wenzao, kama ilivyo hulka ya mwanasiasa yeyote yule mwenye kutaka mamlaka, kama anavyohoji Hansson (2018). Mfano ufuatao unadhihirisha sababu hii;

Dondoo 3: Msemaji 2

> …Mimi nataka niwaambie hii mafuta inaongezwa usiku na mchana, mimi nataka *niwaambie these people don't know the damage they are doing to the people and the economy of the Republic of Kenya*… kwa hii taxes wanaongeza usiku na mchana. Na mimi nataka kuwaambia watu wa hapa Manga tafadhali, mkiona tumesimama hapa mbele yenu, tunawaambia ya kwamba tutengeneze hiyo serikali inayokuja ambayo inaelewa lugha ya mwananchi wa kawaida…
> https://youtu.be/CP_lUfya-s0?si=wn8nnf_puL1oaq9t.
> *Tarehe 1 Agosti, 2022.*

Msemaji anaonekana kutoa lawama kwa serikali ya Uhuru Kenyatta, ambayo pia alihudumu kama naibu wa Rais. Katika muktadha huu, anaonekana kuonyesha kuwa yeye sio mshiriki wala hakuwa na uhusiano na serikali hiyo. Ingawa maoni ya Monge & Lazacano (2022) yanahakikisha kuwa bei ya bidhaa duniani ilipanda baada ya janga la UVIKO-19, msemaji anaonekana kujiepusha na ufahamu wa mfumko wa bei, na badala yake anailaumu serikali ya Uhuru Kenyatta kwa kupandisha bidhaa hizi bei kwa kupenda kwake. Kwa namna hii, anaonekana kuwaeleza wananchi kuwa yeye hakuwa lawamani na kwamba wamwone kama suluhu kwa matatizo hayo. Msemaji anatoa lawama kuhusu kupandishwa kwa bei ya mafuta na serikali, bidhaa muhimu ambayo huathiri sekta nyingi za kiuchumi. Anaendeleza kuwa mbali na serikali kuongeza bei ya bidhaa muhimu, vilevile ilikuwa inaongeza ushuru kwa wananchi wa taifa la Kenya. Anamithilisha haya na serikali kutoelewa lugha ya mwananchi wa kawaida, na kujipigia upato kuwa yule ambaye angeweza kusuluhisha matatizo hayo. Kwa namna isiyo wazi, anajivutia mamlaka kupitia kuwalaumu wapinzani. Lawama zaidi zinatolewa na William Ruto katika kujitafutia uungwaji mkono kutoka kwa wananchi, kama inavyojitokeza ifuatavyo;

Dondoo 4: Msemaji 2

> … Mnajua hawa majamaa, kwa nini wameacha hii bei ya unga mpaka imepanda, ni kwa sababu kitendawili na wenzake hawajawahi kulala njaa … hawajui kulala njaa ni nini. Ata sahii tunaongea bei ya unga, hawajui tunaongea nini… bei ya mbolea ilikuwa shilingi elfu mbili na mia nane, sahii watu wa handshake mbolea wanauza shilingi elfu sita... gorogoro ilikuwa shilingi hamsini, sai gorogoro ni mia mbili… hawa watu wameharibu uchumi wetu ama hawajaharibu…
> https://youtube.com/shorts/bf4OycacI-M?si=NU6wh__XJdDl7iDN.
> *Tarehe 19 Julai, 2022.*

Msemaji anajitokeza kuwalaumu Uhuru Kenyatta na Raila Odinga kwa sababu ya ongezeko la bei ya bidhaa iliyoshuhudiwa kati ya miaka ya 2020-2022. Ingawa duniani kote bei ya bidhaa hizi iliongezeka, msemaji anasisitiza kuwa ilikuwa warejelewa, ambao walikuwa wapinzani wake, ndio waliosababisha bei ya bidhaa alizotaja kupanda. Huku akijiegemeza katika itikadi yake ya Bottoms-up, iliyosisitiza kuwa serikali iliyoongozwa na nasaba za kisiasa haikuwa inawajali maskini, anaeleza kuwa masaibu mengi yaliyowakumba wakenya; yaliwakumba kwa kuwa viongozi wa taifa hawakuwahi kupitia masaibu hayo, kama kulala njaa, kwa hivyo hawakujua la kufanya ili kuhakikisha kuwa wananchi wamepata shibe. Kwa namna isiyo ya moja kwa moja, msemaji anajitwika kiatu cha mwananchi wa kawaida, kwa kujionyesha kuwa pia yeye aliwahi kupitia masaibu kama waliyopitia, kama kulala njaa. Vilevile, msemaji anadokeza ulinganisho wa jinsi bei ya bidhaa ilivyokuwa awali kabla ya kuongezwa na 'nasaba za uongozi wa serikali'. Ili kuridhisha matakwa yake, alitaka kukoleza lawama hizi katika fikra za wananchi, kwa kuwalaumu Uhuru Kenyatta na Raila Odinga kwa kupandisha bei ya bidhaa kama mbolea na mahindi. Kwa kufanya hivi, alilenga kuonyesha kuwa Uchumi wa taifa la Kenya ulikuwa umeporomoka kwa sababu ya viongozi hawa wawili waliohusika katika mkataba wao wa Handshake, na ambao vilevile walikuwa viongozi wa mrengo wa Azimio la Umoja. Katika mchakato huu, msemaji anajivutia mamlaka kwa kuwatia doa wapinzani wake kuhusu maswala tajwa.

### 4.3. Kuwatolea wananchi ahadi

Hulka ya kuwatolea wananchi ahadi ni kawaida kwa mwanasiasa yeyote yule. Itikadi mbalimbali pamoja na hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii huongoza matakwa ya mwanasiasa ya kujivutia mamlaka (Harrison & Boyd, 2018), na hivyo humbidi kutumia mbinu mbalimbali kama suluhisho kwa hali hizo mbalimbali. Mojawapo kati ya mbinu hizi ni utoaji wa ahadi kwa wananchi wasikilizaji. Kwa mujibu wa Panova (2008), ni itikadi ya kisiasa kwa vyama mbalimbali kuongozwa na ahadi ya mambo ambayo watawafanyia wananchi iwapo wangechaguliwa kuongoza serikali. Ahadi hizi hutolewa kwa ushindani wa aina yake, huku kila chama kikitoa ahadi ambazo zilionekana kuwavutia wananchi, ili vyama hivi vipate uungwaji mkono. Wanasiasa hutoa ahadi kuhusu hali ya maisha kuboreka, uchumi kuboreka, kazi kupatikana kati ya wananchi, kupunguka kwa umaskini, elimu kutolewa bila malipo, viwango vya huduma za kiafya kupanda, akina mama kupata nafasi katika uongozi wa serikali na kadhalika. Aghalabu, yale ambayo huahidiwa huhusu yale ambayo yanakumba jamii kwa kipindi fulani. Katika midahalo ya siasa za 2022 nchini Kenya, wanasiasa walitumia itikadi zao za vyama na mirengo yao ya kisiasa kuunda manifesto za vyama hivyo zilizoongoza ahadi ambazo walilenga kuwawasilishia wananchi kuhusu matakwa yao, ili kupata mamlaka. Ahadi hizi zikawa ndio

msingi wa kampeni za wanasiasa hawa, kama ilivyo katika mfano ufuatao;

Dondoo 5: Msemaji 3

> …mwafrika achukue hatamu tupigane na maadui yetu matatu…. ugonjwa, ujinga na umaskini…Kuanzia tarehe tisa mwezi wa nane, tutaanza mwenendo tofauti…. kila mtoto ambaye ame-zaliwa hapa Kenya…atapata fursa sawa ya elimu, kuanzia Nursery, Primary, Secondary, Tertiary mpaka chuo kikuu…. akishamaliza masomo, apate kazi ya maana… Wale ambao wanataka kuanzisha biashara yao wenyewe watapata mkopo kutoka kwa hazina ya serikali na hawalipi chochote mpaka baada ya miaka saba… gharama ya maisha itarudi chini…. bei ya stima na bei ya bidhaa zote muhimu utarudi chini…
> https://youtu.be/9G5YLKeXJ5M?si=Y9-qg1KbS8dBq_Ov.
> *Tarehe 5 Machi, 2022.*

Katika diskosi hii, msemaji anazungumzia kuhusu ahadi ambazo analenga kuwatimizia wananchi iwapo atachaguliwa kuwa rais wa Kenya. Anaangazia kuwa kwa miaka 58 tangu Kenya kujinyakulia uhuru, matatizo ya ugonjwa, umaskini na ujinga zilikuwa zingalipo, na kwamba alikuwa na mipango kabambe ya kusuluhisha matatizo hayo iwapo angepewa nafasi ya kuongoza. Anatoa ahadi kuwa pindi tu baada ya kushinda urais wa Jamhuri ya Kenya, angehakikisha kuwa elimu kuanzia viwango vya chini hadi vyuo vikuu ingefanywa kuwa bure ili kila mkenya apate nafasi ya kuelimika. Vilevile anatoa ahadi kuwa wananchi waliotaka kuanzisha biashara wangepewa fedha za kuhakikisha kuwa wamefanya hivyo, chini ya mpango wa serikali yake, na kwamba pesa hizo zingelipwa baada ya kunawiri kwa biashara hizo. Anagusia kuhusu gharama ya Maisha ambayo ilikuwa imepanda mno kwa kutoa ahadi kuwa gharama hiyo ingerudi chini ili kuwawezesha wananchi wa kiwango cha chini kiuchumi kumudu gharama hiyo. Anataja baadhi ya bei alizopanga kuwa zingerudi chini, kama bei ya huduma ya kawi pamoja na bei ya vyakula nchini. Utafiti huu ulibaini kuwa msemaji aliangazia kusuluhisha baadhi ya shida zilizowakumba wananchi katika wakati huo wa kampeni za uchaguzi, ili kuwafanya wamuunge mkono na kumchagua katika uchaguzi. Mbali na ahadi zilizoangaziwa, kiongozi wa mrengo wa Kenya Kwanza, William Ruto, chini ya mwavuli wa itikadi yake ya Bottoms-Up, alitoa lukuki ya ahadi kwa wananchi wa kipato cha chini na wale maskini kama ifuatavyo;

Dondoo 6: Msemaji 2

> …safari hii tutaanza huku chini ... saa hizi tuongee ya mama mboga, watu wa mkokoteni, mtu wa kinyozi, mtu wa wheelbarrow, mtu wa butchery, mtu ya kiosk...Safari hii tutaweka pia milioni mia moja kila mwaka, kupatia mama mboga, mtu ya kiosk, yule wa mkokoteni na wheelbarrow, pia hao waweze kufanya biashara … Kwa sababu pia nyinyi mnalipa ushuru…kwani pesa ya serikali ikiletwa hapa iko makosa?
> https://youtu.be/wKhiR1UTJ9g?si=sWrcMDao_tHa0bIB.
> *Tarehe 5 Mei, 2022.*

Katika diskosi hii, msemaji anaongozwa na itikadi ya kimatabaka ya Bottoms-Up ambayo ilisisitiza ujenzi wa jamii mpya kiuchumi ambayo ingeanzia chini ikielekea juu. Katika diskosi yake, aliwaangazia hasa wale waliodharauliwa na kutoshughulikiwa na serikali, ambazo kwa muda mrefu zimezingatia shida za viongozi na kumpuuza mwananchi wa kawaida, kwa kuwapa ahadi ainati iwapo angechaguliwa kuwa rais wa taifa la Kenya. Hii ndiyo sababu ya kuwapuuza viongozi na watawala, wale waliokuwa katika taaluma mbalimbali kama walimu, madaktari, manesi na kadhalika, na kujikita katika wale waliokuwa maskini pamoja na waliokuwa wanapitia changamoto mbalimbali za kiuchumi: mama mboga, vinyozi, waliomiliki maduka ya kuuza nyama, wenye vibanda vidogovidogo na kadhalika. Karanja (2022), anachagiza kuwa kuibuka kwa itikadi ya kimatabaka kuliibua umaarufu wa kisiasa katika kambi ya William Ruto kwa kuwa alijihusisha na kundi ambalo lilikuwa kubwa sana nchini, la watu maskini, kupitia ahadi alizowapa ambazo zingesaidia katika kuboresha maisha yao.

### 4.4. Kuwapa wananchi matumaini

Kuzua matumaini ni hulka ya mwanasiasa anayejinadi kwa wananchi. Matumaini huleta hisia ya matarajio na hamu ya jambo fulani kutokea. Baadhi ya wanasiasa katika kampeni za uchaguzi wa 2022 nchini Kenya walihusika katika kuzua hisia hizi za matarajio ya mema kati ya wananchi ambao walikuwa wanakumbwa na matatizo si haba, kijamii na kiuchumi. Kwa namna isiyo wazi, wanasiasa walilenga kuvuta mamlaka upande wao kwa kulenga makundi ya kijamii ambayo yangeafikia matakwa yao. Lindroth & Sineyaraara (2019), wanaeleza kuwa kuwepo kwa dunia isiyoweza kutabirika kunahitaji mwanga ulio na matumaini na ahadi ya upya wa hali na usoni bora. Maoni zaidi yanatolewa na Sacks (1997), ambaye anaeleza kuwa siasa zinazoongoza hasa ni zile ambazo wanasiasa hutumia matumaini kama chambo, huku wakipata uungwaji mkono kutoka kwa wananchi kwa sababu ya kuwapa matumaini. Anaeleza kuwa makundi fulani hulengwa kwa minajili ya kupewa matumaini haya. Mfano ufuatao unafichua hali hii;

Dondoo 7: Msemaji 3

> … Kuna vikundi vingine vya akina mama ambao wana watoto na hawana mabwana…hawa wamama wanapata shida nyingi sana.... watapata msaada kutoka kwa serikali yangu... ni mwanzo mpya, tuaanza mwanzo mpya…
> https://youtu.be/9G5YLKeXJ5M?si=Y9-qg1KbS8dBq_Ov.
> *Tarehe 5 Machi, 2022.*

Diskosi hii inadhihirisha matumaini kwa kundi la akina mama lenye watoto ila wasio na waume wanaowalea wana wao. Kwa mujibu wa takwimu za Kenya Demographic and Health Survey, familia zinazoongozwa na mzazi mmoja, hasa mwanamke, ziliongezeka sana kwa miaka 10 iliyopita, kabla ya mwaka wa 2020; kutoka asilimia 25 hadi 38. Familia hizi hukumbwa na matatizo ainati, za kijamii na kiuchumi, kwa mfano, ukosefu wa chakula, karo ya Watoto,

ukosefu wa mahitaji ya kimsingi katika familia na kadhalika. Maoni zaidi yanatolewa na Igandu (2023), kuhusu changamoto zinazowakumba akina mama walio katika hali hii. Anaeleza kuwa changamoto hizi, nyingi zikiwa za kiuchumi, huwa mzigo mzito kwa akina mama hawa, ambao huendelea kuteseka kwa kukosa mahitaji maalum ya kukidhi haja za watoto wao. Katika diskosi hii, msemaji anaonekana kukubali kuwa kundi hilo lipo. Anaeleza kuwa kundi hilo hukumbana na changamoto nyingi sana, na kuwapa tumaini kuwa watapokea msaada kutoka kwa serikali yake, iwapo angefanikisha azma yake ya kuwa rais wa taifa la Kenya. Msemaji anaita hali ya kuwajali akina mama hawa kama mwanzo mpya, ikizingatiwa kuwa hakuna serikali yoyote nchini ambayo imewahi kuwasaidia akina mama kama hawa katika kukidhi mahitaji yao ya kimsingi ya kila leo. Greene & Elder (2012), wanadhihirisha uwepo wa siasa katika hali ya familia za mzazi mmoja. Wanaeleza kuwa viongozi wa kisiasa hawana budi kutoa maoni kuhusu familia kama hizi, kwa nia ya kujiongezea ushawishi wa kisiasa. Ikirejelewa kuwa familia hizi zimeongezeka sana katika mwongo uliopita, msemaji anazungumza kwa ufahamu wa idadi hii na kwamba analenga kupata uungwaji mkono kutoka kwa kundi hili. Hii ndiyo sababu yake kuwapa tumaini akina mama walio katika kundi hili, ili kujipatia umaarufu kati yao kwa minajili ya kujivutia mamlaka.

Eldelman (1977), anaeleza kuwa suluhu kwa umaskini unaokumba jamii ni matumaini. Anaeleza kuwa lugha ya kisiasa inapaswa kuangazia matatizo yanayowakumba wananchi maskini kwa kujaribu kudhihirisha suluhu kwa matatizo hayo. Matumaini hayo yanapaswa kutiliwa nguvu na mwanasiasa ili kuonekana kuwa ya kweli, ingawa matumaini hayo huibuka bila uhalali wa iwapo yatatendeka au la. Hii ndiyo sababu ya wananchi wengi maskini kupewa matumaini kwa wingi na wanasiasa wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2022. Raila Odinga anaonekana kuwapa wananchi maskini matumaini katika diskosi ifuatayo;

Dondoo 8: Msemaji 3

> … Kuna wengine wetu hawana mapato ata kidogo, wanaitwa hohehahe...Tutaleta Social Welfare Program hapa Kenya, Ile jamii ambayo hawana chochote wapate kila mwezj shilingi elfu sita…
> https://youtu.be/0sflLHYdkFk?si=aG4TJRQXklq-0Z5j.
> *Tarehe 8 Julai, 2022.*

Msemaji anadhihirika kuwapa matumaini wananchi maskini nchini Kenya. Kwanza, anakubali kuwa wananchi wengi ni maskini hohehahe kwa sababu waliishi kwa kipato kidogo. Kwa sababu hii, anawapa tumaini kuwa baada yake kuchaguliwa kuwa rais, basi wangepata shilingi elfu sita kila mwezi ili kuwakwamua kutoka katika changamoto ya kukosa kipato.

## 4.5. Kuchochea dhidi ya wapinzani

Baadhi ya diskosi za wanasiasa zilidhihirisha uchochezi dhidi ya wapinzani. Uchochezi huo ulionekana kuegemea dhidi ya viongozi fulani wa upinzani. Waliochochea walilenga kuwafanya wananchi kuchukizwa na wanasiasa fulani; hivyo kuwakataa. Walichochea ili kujivutia mamlaka, kwa kuonekana kudhibiti fikra na matendo ya wananchi, kwa kuwataka wafanye walivyowataka kufanya, bila kuwashurutisha kwa njia yoyote. Zeitzoff (2023), anazingatia siasa chafu kwa kueleza kuwa siasa ni ulingo wenye uchafu na ambao umejaa visa vingi vya matusi na uchochezi dhidi ya wapinzani. Anaeleza kuwa wanasiasa wachochezi hudhamiria kuwadharau wapinzani kupitia diskosi zao kwa njia ambayo itawafanya wananchi vilevile kuiga matakwa yao, hivyo kuwaangusha katika siasa. Kwa njia fiche, wachochezi hutumia fursa hiyo kujivutia mamlaka upande wao huku wakiwapokonya mamlaka wapinzani wao. Isitoshe, uchochezi huo huambatana na matusi ya kudhalilisha kwa nia ya kuharibu azma ya wapinzani kisiasa huku wenyewe wakijikuza. Mfano ufuataoo unadhihirisha hali hii;

Dondoo 9: Msemaji 2

> …Koyai ko kimnyige ak anyun ne, ogoik chebo Kesses, ogoik? Chi ne pilipili nyonei kotinyei, ogoik? Ogoik, acham ak ogoik akeng' ne miech. Acha matinye ak maibee tugul Kalenjin. Chi ne kotinyei kura, ak anyun ak kongoi ak nyonei konyonei chebo pesa ne bo ng'uni? Mocha chi noto tugul; maacham chi ne kotinyei Nairobi ak kongoi amun kuting'ei chi age, ak kotinyei Nairobi ak chepchin ak konyonok chebo konyikto ne miech, kora ak koboit ne ak kongoi amun ma bo kitu…Tugul ne bo age nyonei? Amun itinyei deni chebo chi ne pilipili? Amun koit ne? Maacham tugul Kalenjin… ak kongoi amun ko nyonei. Barabarik chebo ak atilil ko kilomita 1400, amun ak kewendi kongoi amun ak anyun Kalenjin? Chi ne kora kiech ak kitinyei ak kimochei chi noto, ak chi noto anyor amun akany, kora ko kiptai tugul. Amun maing'ei?
> Ogoik chebo ne?

Tafsiri

> …Mko na mchawi mwingine hapa msikie watu wa Kesses, mnasikia? Mtu wa pilipili aende nyumbani, mmeskia? Mskie, nataka mnisikilize vizuri, sitakii mwaibishe jamii ya Kalenjin. Mtu mwenye alipewa kura, kufika huku akasema alinunua, aliwanunua na pesa ngapi? Msahau huyo mtu kabisa, hatutaki mtu mwenye akifika Nairobi anasema hakuna watu, akifika Nairobi anashikana na maadui ndio watuue na akirudi huku anasema sio kitu…ni jamii gani ilinunuliwa? Mko na madeni ya mtu wa pilipili? Anawadai? Hatutaki jamii yetu ya Kalenjin… isemekane huwatunanunuliwa… Barabara ambazo nimejenga ni karibu kilomita 1400, lakini nimewahi kusema nimenunua Wakalenjin? Mtu mwenye tulimheshimu tukampea kitu mtu akakua mjinga, na sahii anatuangusha, hapana haiwezekani? Watu wa hapa mnaskia? https://youtu.be/2tALstWfq5I?si=VojiUrtDrow0WYCs.
> *Tarehe 25 Julai, 2022.*

Msemaji anawachochea wananchi wa Kesses dhidi ya mbunge wao (2017-2022), Mheshimiwa Mishra. Anamrejelea kama "mtu wa pilipili" kwa kuwa Wahindu wengi huwa na hulka ya kupenda vyakula vilivyokolezwa kwa pilipili (Srinivas, 2011). Vilevile, anamrejelea kwa jina "mchawi", neno ambalo linaonekana kama tusi dhidi

ya mrejelewa. Msemaji anaonyesha kupitia diskosi hii udhibiti wa kifikra na kitabia dhidi ya mlengwa. Anawadhibiti wananchi wa Kesses kwa kuwataka wasimchague mwanasiasa Mishra. Anawaeleza kuwa hakuwataka waaibishe jamii yao ya Kalenjin kwa kumchagua kiongozi mhindu. Msemaji vilevile anawaeleza sababu za kutowataka kumchagua kiongozi huyo, mojawapo ikiwa kutoa madai kuwa kiongozi huyo alijitapa kuwa aliwanunua wana eneo-bunge hilo. Anajivutia mamlaka kwa kuwaeleza yote ambayo amewatendea bila kudai kuwa alikuwa amewanunua, hivyo kuonekana kuwa aliyehitajiwa zaidi ya mrejelewa. Kwa njia isiyo wazi, msemaji anawadhihirishia wananchi wa Kesses kupitia uchochezi kuwa hawakumhitaji mrejelewa kwa njia yoyote bali walimhitaji yeye pamoja na kufuata matakwa yake binafsi ili waweze kufanikiwa kama eneo bunge.

Mfano mwingine wa wanasiasa kuchochea huku wakidhihirisha mamlaka katika diskosi zao ulidhihirika kupitia hotuba ya William Ruto mjini Tana River;

Dondoo 10: Msemaji 2

> …Kiongozi yeyote ambaye amepiga kura yes kwa BBI ati pesa ya Tana River ipunguzwe asichaguliwe…mimi nawaambia, kiongozi yeyote anayechaguliwa, anachaguliwa kwenda kulinda haki ya waliomchagua… kama kiongozi anachaguliwa, anafika Nairobi, anafika Hola, anauza haki ya wale walimchagua, huyo sio kiongozi, huyo ni tapeli…
> https://youtu.be/icrNuvwm5Cc?si=ivsSBnaR_y1Ypa7k.
> *Tarehe 12 Januari, 2022.*

Msemaji anawachochea wananchi dhidi ya baadhi ya viongozi wa eneo la Tana River, walio wabunge wa kitaifa na wale wa maeneo gatuzi. Onguny (2020), anaeleza kuwa mchakato wa Building Bridges Initiative (BBI) uliibuka miongoni mwa wanasiasa wa mrengo wa Azimio la Umoja, huku wakinuia kuleta mabadiliko katika katiba ya nchi ya Kenya. Mojawapo kati ya yale ambayo yangebadilishwa ni ugavi wa raslimali kati ya wakenya, huku mchakato huu ukipendekeza kuwa maeneo yenye watu wengi yangepokea pesa zaidi za serikali ikilinganishwa na yale maeneo yaliyokuwa na watu wachache. Msemaji alichukua fursa ya kuwatembelea wananchi wa Tana River, sehemu mojawapo iliyokisiwa kuathirika pakubwa iwapo mchakato wa BBI ungefaulu kupita, ili kuwachochea dhidi ya viongozi wao ambao walihusika katika kupitisha mchakato huo kupitia kura katika mabunge yao (Karanja, 2022). Anawaeleza wananchi kuwa wasiwapigie kura wale viongozi ambao walipitisha mchakato huo. Anawakumbusha kuwa badala ya viongozi hao kutetea maswala ya wananchi hao, walihusika katika kuhakikisha kuwa wananchi wenyewe wasingepata raslimali ya kutosha kutoka kwa serikali. Anawachochea kwa kuwaeleza kuwa kwa sababu viongozi hao walihusika katika kuwanyang'anya haki wananchi hao, basi hawakuwa wananchi bali walikuwa matapeli. Maelezo ya msemaji yanadhihirika kuwa yenye shuruti, kwani anawaamrisha wananchi hao kufanya kulingana na matakwa yake. Kwa namna hii, anawadhibiti wananchi hawa hivyo kudhihirisha mamlaka upande wake huku akiwapokonya mamlaka wale viongozi ambao waliunga mkono mchakato wa BBI.

### 4.6. Kufanikisha propaganda zao

Propaganda ni jambo la kawaida katika siasa ambalo huwa ni jitihada za makusudi za kueneza Habari, Mawazo au itikadi – mara nyingi zikiwa na upendeleo au kupotosha – ili kushawishi maoni, hisia na tabia za jamii kuelekea upande fulani, hasa wa kisiasa. Mugaduka & Murithi (2023), wanahoji kuwa diskosi huongozwa na maswala kadhaa, yakiwemo historia na itikadi. Wanaeleza kuwa diskosi huongoza imani. Wanachagiza kuwa propaganda hujitokeza kama maelezo yasiyo yenye uaminifu ila yamehalalishwa ili kukidhi haja za mwanasiasa ama mmiliki wa diskosi. Maelezo haya yanapotolewa mbele ya wananchi wapigaji kura, huwaathiri kitabia na kiakili. Katika harakati hizi, hali ya utousawa husababishwa kati ya makundi ya kisiasa, hivyo kusababisha mwanasiasa fulani kujivutia mamlaka kwa njia isiyo wazi. O'Shaughnessy (2024), anaeleza propaganda kama silaha ya kuangamiza umma. Anaeleza kuwa siasa inapohusishwa na propaganda huwa na athari hasi mno katika maisha ya wanajamii. Husababisha wananchi kufanya maamuzi kulingana na maelezo yasiyo ya kweli, au yaliyotiliwa chuku, hivyo kuyafanya maamuzi hayo ya wananchi kuwa yasiyofaa. Maelezo zaidi yanatolewa na Chapman (2000), ambaye anatathmini propaganda kuwa silaha ya kisiasa yenye nguvu zaidi, ingawa huwa maelezo yasiyo na msingi. Wananchi wanapopewa propaganda, baadhi yao huamini maelezo hayo, hivyo kuathirika kifikra. Isitoshe, kwa kuwa propaganda hulenga kuwaathiri wapinzani kwa njia hasi, wamiliki hufaidika kwa kujivutia mamlaka kwa njia isiyo ya moja kwa moja, huku walengwa wakitwazwa kwa maelezo yasiyo na msingi. Hivyobasi, propaganda huleta faida kwa wengine huku wapinzani wakipata hasara kisiasa.

Katika midahalo ya siasa za uchaguzi mkuu wa 2022 nchini Kenya, baadhi ya wanasiasa walidhihirisha mamlaka kwa nia ya kufanikisha propaganda zao. Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii;

Dondoo 11: Msemaji 2

> ……hiyo program yetu haikufaulu kwa sababu yule mtu wa kitendawili alitutembelea na akalete kisirani…akakuja akatuambia kwamba mambo ya kupanga ajira ya hawa vijana siyo ya maana, akasema twende tubadilishe katiba tuweke vyeo vya viongozi, tuongeze mamlaka ya viongozi na tutengeneze formula ambayo inahujumu watu wa Tana River… https://youtu.be/CT74OMceDkQ?si=tiXX6dKKPAho5xIe.
> *Tarehe 4 Januari, 2022.*

Diskosi hii inadhihirisha propaganda. Msemaji, William Ruto anaeleza kuwa mipango waliyopanga na Uhuru Kenyatta ilisambaratika kwa sababu Raila Odinga alijiunga na serikali kupitia maridhiano aliyofanya na Uhuru Kenyatta almaarufu kama The Handshake. Hakuna ithibati aminifu inayoweza kutolewa ili kudhibitisha kuwa Raila Odinga alisema kuwa ajira ya vijana haikuwa ya maana. Vilevile, hakuna ithibati kuwa sehemu ya Athi

River ilikuwa akilini mwa Raila Odinga alipopendeeza fomula ya ugavi wa raslimali kutumika kupitia mchakato wa BBI. Kwa mwananchi wa kawaida asiye maanani, basi huyo mrejelewa, Raila Odinga, alikuwa adui mkubwa aliyelenga kuhujumu mustakabali wa mwananchi wa Tana River. Kwa kutoa maelezo haya, msemaji alilenga kujivutia mamlaka kwa njia isiyo wazi huku akimtwaza Raila Odinga, ambaye anamrejelea kama "mtu wa kitendawili."

## 5. Hitimisho

Uchanganuzi huu umedhihirisha kuwa mwanasiasa huongozwa na malengo fulani kila anapotumia mamlaka na itikadi za kisiasa katika diskosi zake. Lugha imejitokeza kama chambo cha kudhihirisha malengo. Kupitia matumizi angavu ya lugha, iliyosukwa kwa njia ya aina yake, vipashio vya mamlaka hubainika huku itikadi mbalimbali za kisiasa zikidhihirika hasa kupitia maneno ya lugha. Itikadi hizi huongoza imani ya mwanasiasa pamoja na mielekeo ya wasikilizaji, hivyo kuathiri maamuzi yao. Malengo ya wanasiasa huambatana na matakwa yao. Hii ndiyo sababu ufanisi wa diskosi zao hupimwa kulingana na udhibiti waliofanikisha kati ya wananchi. Kwa kuwadhibiti wananchi, huafikiana na malengo yao na sababu zao za kutumia mamlaka. Kwa kutamatisha, mamlaka na itikadi zinajitokeza kuwa dhana zisizoibukia katika ombwe tupu, bali hubainika kwa malengo maalum.

## Marejeleo


Bevir, M. (1999). Foucault, power, and institutions. Political studies, 47(2), 345-359.

Brown, G., & Yule, G. (1983). Discourse analysis. Cambridge university press.

Chapman, J. (2000). The power of propaganda. Journal of Contemporary History, 35(4), 679–688. https://doi.org/10.1177/002200940003500410

Edelman, M. (1977). The language of participation and the language of resistance. Human Communication Research, 3(2), 159–170.

Fairclough, N. (1989) Language and power. London: Longman.

Fairclough, N. (1993). Critical discourse analysis and the marketization of public discourse: The universities. Discourse & society, 4(2), 133-168.

Fairclough, N. (2001). Critical discourse analysis as a method in social scientific. Methods of critical discourse analysis, 113, 121.

Fairclough, N. (2003). Analysing discourse (Vol. 270). London: routledge.

Fairclough, N. (2006). Genres in political discourse. JL Mey, concise encyclopedia of pragmatics, 293-298.

Greene, S., & Elder, L. (2012). The politics of parenthood: Parenthood effects on issue attitudes and candidate evaluations in 2008. American Politics Research, 40(3), 419–449.

Hansson, S. (2018). Analysing opposition-government blame games: Argument models and strategic maneuvering. Critical Discourse Studies, 15(3), 228–246.

Harms, J. (2021). Disrupting ethnic politics and imagining alternative futures in Kenya, 1975: The J. M. Kariuki assassination (Doctoral dissertation, University of British Columbia).

Harrison, K., & Boyd, T. (2018). The role of ideology in politics and society. In Understanding political ideas and movements (pp. 135–153). Manchester University Press.

Igandu, L. A., Odek, A., & Marima, E. (2023). Single parenting and children's academic performance in primary schools in Embu East Sub County, Kenya. African Journal of Empirical Research, 4(2), 916–928.

Jones, J., & Peccei, J. S. (2004). Language and politics. In L. Thomas (Ed.), Language, society and power. Routledge.

Karanja, J. M. (2022). 'Hustlers versus Dynasties': contemporary political rhetoric in Kenya. SN Social sciences, 2(10), 230.

Kress, G. (1990). Critical discourse analysis. Annual Review of Applied Linguistics, 11, 84–99.

Kress, G. (2003). Visual and verbal modes of representation in electronically mediated communication: The potentials of new forms of text. In I. Snyder (Ed.), Page to screen: Taking literacy into the electronic era (pp. 53–79). Routledge.

Ku, A. S. (1998). Boundary politics in the public sphere: Openness, secrecy, and leak. Sociological Theory, 16(2), 172–192.

Lindroth, M., & Sinevaara-Niskanen, H. (2019). Politics of hope. Globalizations, 16(5), 644–648.

Monge, M., & Lazcano, A. (2022). Commodity prices after COVID-19: Persistence and time trends. Risks, 10(6), 128.

Mugaduka, M. S., & Murithi, J. (2023). Itikadi katika tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004). Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 6(1), 84–100.

Onguny, P. (2020). The politics behind Kenya's Building Bridges Initiative (BBI): Vindu vichenjanga or sound and fury, signifying nothing? Canadian Journal of African Studies, 54(3), 557–576.

O'Shaughnessy, N. (2024). Politics and propaganda: Weapons of mass seduction.

Panova, E. (2008). Campaign promises and political factions. Cahier de Recherche/Working Paper, 8, 1-20.

Patton, M. Q. (2002). Qualitative research and evaluation methods (3rd ed.). Sage Publications.

Sacks, J. (1997). The politics of hope.

Srinivas, T. (2011). Exploring Indian culture through food.

Education About Asia, 16(3), 38–41.

Van Dijk, T. A. (1984). Prejudice in discourse: An analysis of ethnic prejudice in discourse. John Benjamins Publishing.

Van Dijk, T. A. (1998). Ideology: A multidisciplinary approach. Sage.

Wodak, R. (1996). Critical linguistics and critical discourse analysis. Handbook of Pragmatics. Benjamins.

Wodak, R. (2001). What CDA is about: A summary of its history, important concepts and its developments. In R. Wodak & M. Meyer (Eds.), Methods of critical discourse analysis (pp. 1–13). Sage.

Wodak, R. (2004). Critical discourse analysis. Qualitative research practice, 185, 185-204.

Wodak, R. (2009). The discourse of politics in action: Politics as usual. Sage.

Zeitzoff, T. (2023). Nasty politics: The logic of insults, threats, and incitement. Oxford University Press.